HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 KWA KUTUMIA MAPATO YA NDANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU Januari – Machi 2019.**









**IMEANDALIWA NA;**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W) LONGIDO DC.**

**March 2019.**

**YALIYOMO.**

**YALIYOMO**……………………………………………………….......	i

**ORODHA YA MAJEDWALI** ………………………………...............	i

**ORODHA YA PICHA**…………………………………………………..	i

**UTANGULIZI**……………………………………………………........	1

1.1. Sekta ya Mipango…………………………………………………..	1-2

1.2 Sekta ya Afya…………………………………………………………	3

1.3 Sekta ya Elimu Sekondari……………………………………………	3

1.4 Sekta ya Mifugo………………………………………………………	4

1.5 Sekta ya Usafi na Mazingira…………………………………………	4

**2.0 CHANGAMOTO**…………………………………………………	5

2.1 Utatuzi wa Changamoto……………………………………………..	5

**ORODHA YA PICHA.**

1.1 Picha inayoonyesha hatua za Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Noondoto kwa muonekano wa mbele na pembeni…………………………………………………… 2 - 3

1.3 Picha kuonyesha ujenzi wa madarasa mawilin(2) na ofisi moja katika kijiji cha Engarenaibor…………………………………………………… 2

**ORODHA YA JEDWALI.**

1.1 Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2018/19……………………………………………….. 6 - 8

## UTANGULIZI.

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido ilitenga kiasi cha Tsh. 77,781,904 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo iliyopangwa katika sekta ya Mipango, Afya, Elimu sekondari, Mifugo, Usafi na mazingira. Matumizi yalikua ni Tsh 77,781,904 na hakuna fedha iliyobaki kama ilivyoainishwa hapa chini;

### 1.1 IDARA YA MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI.

Halmashauri ya Wilaya ya Longido iliweka Bajeti Jumla ya **Tsh.51,789,700/=** kwa Idara ya mipango na kati ya fedha hizo Halmashauri iliidhinisha jumla ya **Tsh. 36,268,154** kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizopangwa katika sekta hiyo kama inavyoonesha katika mchanganuo ufuatao;

a) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika vijiji 49 kufikia juni 2019.

Halmashauri ilitenga na kutumia jumla ya **Tsh 8,705,000** kwa ajili ya kutembelea miradi inayotekelezwa katika kata zote 18 ili kuangalia thamani ya fedha(Value for Money) ya miradi hiyo. Miradi yote imetembelewa na mapendekezo yametolewa kwa miradi husika ili miradi iweze kuwa na tija kwa jamii.

b) Kufanya Uchambuzi yakinifu (Feasibility Study) wa Miradi ya Kimkakati.

Halmashauri ilitenga na kutumia jumla ya **Tsh 20,000,000** kwa ajili ya kuibua miradi ya kimkakati katika kata ya Kimokouwa ikiwa ni pamoja na; Ujenzi wa Stendi ya Malori na Ujenzi wa soko la Mazao Eorendeke. Andiko la Maegesho limeshawasilishwa OR-TAMISEMI na andiko la Soko la uandaaji wa Hati Miliki unaendelea.

c) Kukamilisha miradi 5 ya Maendeleo Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Halmashauri ilitenga na kutumia jumla ya **Tsh 7,563,154** kwa ajili ya kuunga juhudi za Nguvu za Wananchi katika kukamilisha ujenzi wa ofisi ya kata ya Noondoto. Jengo hilo la ofisi tayari limekamilika kwa sehemu kubwa kwani upauzi tayari,milango na madirisha pia tayari,na liko hatua ya kukamilisha ujenzi na kuanza kutumika.



*Picha 1.1 :Hatua za Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Noondoto kwa Hatua iliyofikiwa kwa muonekano wa pembeni.*



*Picha 1.1 :Hatua za Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Noondoto kwa muonekano wa mbele.*

### 1.2 IDARA YA AFYA.

Halmashauri ilitenga fedha jumla ya **Tsh.32,513,750/=** kwa ajili ya miradi ya Afya ambapo jumla ya **Tsh.32,513,750/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Ketumbeine na mchakato wa kuhamisha fedha Akaunti ya Kijiji unaendelea.

### 1.3 IDARA YA ELIMU SEKONDARI.

Halmashauri ilitenga jumla ya **Tsh.94,000,000/=** kwa ajili ya kufanya shughuli zifuatazo;

a) Kuunga mkono nguvu za Wananchi kwa kuchangia ujenzi wa Maabara shule ya Sekondari Matale katika kata ya Tingatinga na Lekule. Fedha bado hazijatolewa.

b) Kumalizia ujenzi wa Chumba kimoja cha Darasa shule ya Sekondari Engarenaibor katika kata ya Engarenaibor. Jumla ya Tsh.9,000,000/= zimehamishiwa kwenye Akaunti ya shule na ujenzi umefikia hatua ya Lenta.

c) Kukamilisha ujenzi wa vyumba vya Madarasa na Nyumba za mwalimu kwa shule

za sekondari kwa ajili ya Kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa shule za sekondari katika kata ya Tingatinga na Lekule. Fedha bado hazijatolewa.



*1.3 Picha kuonyesha ujenzi wa madarasa mawilin(2) na ofisi moja katika kiji cha Engarenaibor.*

### 1.4 IDARA YA MIFUGO NA UVUVI.

Halmashauri ilitenga fedha jumla ya **Tsh.18,500,000/=** kwa ajili ya kuboresha mnada wa Orbomba ili kuongeza mapato yatokanayo na mnada,ambapo hadi sasa hakuna fedha zilizotolewa.

### 1.5 IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA.

Halmashauri ilitenga fedha jumla ya **Tsh.20,000,000/=** kwa ajili ya kuweka uzio kwenye dampo kwenye kata ya Kimokouwa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye eneo la Dampo na kuzuia uwezekano wa magonjwa ya Mlipuko. Hakuna fedha zilizotolewa.

## 2.0 CHANGAMOTO.

- Vyanzo vichache vya mapato kwa Halmashauri ya Wilaya
- Miundombinu mibovu ya mawasiliano,barabara na upatikanaji wa mitandao ya simu
- Mwiitikio mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi.
- Fedha kutofika kwa wakati.

## 2.1 UTATUZI WA CHANGAMOTO.

- Ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato.
- Kuomba fedha toka Serikali Kuu kwa ajili ya kuboresha miundombinu Wilayani.
- Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa uchangiaji wa miradi ya Maendeleo.
- Kuishauri Serikali kutoa idhini ya matumizi ya fedha kwa wakati.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI 2018/19 ROBO YA TATU: JANUARI – MACHI 2019**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | | | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S/N | Sekta | Jina la mradi. | Kazi zitakazotekelezwa. | Kata/Kijiji/ Mtaa. | Fedha iliyoidhiniswa | Fedha iliyotolewa | | | Matumizi | Baki | Maelezo. |
| | | | | | | Halmashauri | Wananchi | Wengineo | | | |
| 1 | Mipango Takwimu na Ufuatiliaji. | Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika Vijiji 49 kufikia Juni 2019 | Kuangalia **Value for Money** kwa Miradi inayotekelezwa. | Kata zote 18 | 11,789,700 | 8,705,000 | 0 | 0 | 8,705,000 | 3,084,700.00 | Miradi imetembelewa na mapendekezo yametolewa kwa miradi husika ili miradi iweze kuwa na tija kwa jamii |
| 2 | | Kufanya Uchambuzi yakinifu (Feasibility Study) wa Miradi ya Kimkakati<br><br>1.Ujenzi kwa Stendi ya Malori<br><br>2. Ujenzi wa Soko la Mazao | Kuongeza vyanzo vya Mapato kwa Halmashauri na kuongeza ukusanyaji wa mapato | Kimokouwa | 25,000,000 | 20,000,000 | 0 | 0 | 20,000,000 | 5,000,000 | Andiko la Maegesho limeshawasilishwa OR-TAMISEMI na andiko la Soko uandaaji wa Hati Miliki unaendelea |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Eorendeke | | | | | | | | | |
| 3 | | Kukamilisha miradi 5 ya Maendeleo Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido | Kuunga juhudi za Nguvu za Wananchi katika kukamilisha ofisi ya kata. | Noondoto | 15,000,000 | 7,563,154 | 0 | 0 | 7,563,154 | 7,436,846 | Ungozi wa Kata umehimizwa kukamilisha jengo la Ofisi kwa wakati. |
| 4 | Afya. | Kuunga mkono nguvu za Wananchi katika ujenzi wa Kituo cha Afya Ketumbeine | Kuboresha huduma za Afya kwa kusogeza karibu na Jamii. | Ketumbei ne | 32,513,750 | 32,513,750 | 0 | 0 | | 0 | Taratibu za Kuhamisha fedha zinaendelea kwenda kwenye Akaunti ya Kata |
| 5 | Elimu Sekondari. | Kuunga mkono nguvu za Wananchi kwa kuchangia ujenzi wa Maabara shule ya Sekondari Matale | Kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa shule za Sekondari | Tingatinga na Lekule. | 60,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | | Fedha bado hazijatolewa |
| 6 | | Kumalizia ujenzi wa Chumba kimoja cha Darasa shule ya Sekondari Engarenaibor | Kupunguza uhaba wa vyumba vya Madarasa kwa shule za Sekondari. | Engarenai bor | 9,000,000 | 9,000,000 | 0 | 0 | 9,000,000 | | Fedha zimehamish iwa kwenye Akaunti ya shule na ujenzi umefikia hatua ya Lenta |
| | | Kukamilisha | Kuboresha | Tingatinga | 25,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | | Fedha bado |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | | ujenzi wa vyumba vya Madarasa na Nyumba za mwalimu kwa shule za sekondari. | mazingira ya kujifunzi kwa shule za sekondari | na Lekule. | | | | | | | hazijatolewa . |
| 8 | Mifugo. | Kuaendeleza Mnada wa Orbomba | Kuboresha Minada ya Halmashauri ili kuongeza Mapato | Orbomba | 18.500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | Fedha bado hazijatolewa |
| 9 | Usafi na Mazingira. | Kuweka uzio kwa Dampo la Kimokouwa | Kuimarisha ulinzi kwenye eneo la Dampo na kuzuia uwezekana wa magonjwa ya Mlipuko | Kimokouw a | 20,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | Fedha hazijatolewa |
| | | **JUMLA KUU** | | | **198,303,450** | **77,781,904** | **0** | **0** | **45,268,154** | **15,521,546** | |

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.**

S.L.P 84; LONGIDO DC.

Simu:– Mkurugenzi wa Halmashauri - 255-0655-268-384. Mchumi: 0769020903

Tovuti: www.longidodc.go.tz